

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Ofisi ya Rais

MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII



Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Awamu ya Tatu

Kutangaza Mfumowa Sera ya Makundi Maalum kwenye Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini

1. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Watu wa Marekani (USAID), Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Wizara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DFID), na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Sweden (Sida) yameendelea kusaidia kuchangia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Awamu ya Tatu kutekeleza Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini katika Halmashauri zote Tanzania Bara nawilaya zote Zanzibar.

2. Lengo la Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ni kuziwezesha kaya maskini zinazoishi katika mazingira magumu kufanya shughuli mbali mbali ili kuzinusuru kutokana na majanga ambayo yanaweza kuathiri vipato na rasilimali zao, kuzipatia stadi mbali mbali ili wazitumie katika kujitoa kwenye hali duni na kuboresha hali zao za maisha. Lengo mahsusi la Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ni kuziwezesha kaya maskini kuwa na uwezo wa kupata chakula nakuondokana na keroya umaskini ambayo wameishi nayo kwa muda mrefu. Kupitia Mpango huu, kaya maskini zitaanzisha shughuli za uzalishaji mali ili kujikwamua kiuchumi na hivyo kujitea maendeleo.

3. Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini hutoa ruhusu kwa wakati kwa kaya maskini zilizokidhi vigezo vya umaskini na kuandikishwa kwenye daftari la walengwa. Shughuli zinazotekelezwa na Mpango ni pamojana: (i) kushirikisha kaya na uongozi wa sehemu husika katika utekelezaji wa shughuli zinazowahusu walengwa. (ii) kutoa mafunzo kwa wataalam katika ngazi za Jamii, Halmashauri na Taifa, (iii) kufuatilia utekelezaji na kupima matokeo kama yanaendana na malengo yaliyokusudiwa (v) kuratibu utekelezaji wa shughuli zote zinazofanywa katika Jamii; (vi) kupanga utekelezaji wa shughuli nyingine ndani ya Mpango ambazo zinalinga kuinua hali ya maisha ya kaya maskini (vii) kutoa mchango kwenye utekelezaji wa shughuli zinazofanywa katika jamii ili kuwa na matumizi mazuri ya rasilimali (viii) na kujenga mahusiano na programu nyingine zinazosaidia jamii kujiimarisha kiuchumi.

4. Mpango unakusudia kuzifikia kaya ambazo ni maskini zaidi nchini ikiwa ni pamoja na makundi maalum. Sifa za makundi maalum ni zile kaya ambazo: (i) hazina uhakika wa chakula (ii) zinakosa huduma muhimu za jamii ikiwa ni pamoja na zilezilizokopembezoni(iii) kaya zisizoshirikikwenyeshughulikwenyejamiizao(iv) kaya zilizokosa usawa na uwezo wa kufanyamaamuzikatikajamii.

5. UtekelezajiwaMpangoutahusishakuzingatia Serazakulindawatunamazingirapamojana Sera yamakundiMaalum .MpangowaKunusuru Kaya Maskiniunahudumia kaya milioni 1.1 nchini ambazo hazina uhakika wa chakula. Kati ya hizo, kuna kaya ambazo (i) zinaongozwa na wanawake, watoto au wazee, (ii) kaya zenye idadi kubwa ya watoto na vijana (iii) kaya zenye watu wanaoishi na magonjwa ya muda mrefu kama ukimwi, kifua kikuu nk (iv) kaya zisizoshirikikwenyeshughulikwenyejamiizaonawanaoishikatikamazingira magumu sana kufikika kijografia.

6. Mfumowa Sera hiiumeandaliwakuhakikishakuwakuna uhuru, nawigompanaunaoiwezeshamakundiya maalum kupata taarifa sahihi nakushirikikatikashughulizaMpango; kubaini athari zozote mbaya na kuzipatia ufumbuzi; zinapata manufaa stahiki; kuweka utaratibu wa kushughulikia malamiko, kufanya tathmini na ufuatiliaji kwa makundi hayo.

7. Mfumowa Sera ya Makundi Maalum unatangazwa ili umma upate taarifa na unapatikana sehemu zifuatazo:

Ofisi ya Makamu wa Rais, Kitengo cha Mazingira
Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira
Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Dodoma na Dar es Salaam
Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar
OfisizotezaWakurugenziwa Mamlaka za SerikalizaMitaaTanzania Bara.

Mfumowa Sera ya Makundi Maalum pia unapatikanakatikatovutiya TASAF nakwenyeKituo cha Habari chaBenkiyaDunia(InfoShop).

Maelezo zaidi yanaweza kupatikana kutoka kwa anuani ifuatayo.

Mkurugenzi Mtendaji,
Mfuko wa Maendeleo ya Jamii ,
Barabara ya Kilwa/Malindi
S.L.P. 9381 ,
Dar es Salaam

Simu : +255 22 2123583/4
Nukushi : +255 22 2123582
Barua pepe: info@tasaf.org
Tovuti :www.tasaf.org